

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

Anuani ya Simu: "UTUMISHI" Dar es Salaam  
Simu Na: +255 22 2118531/4  
Nukushi: +255 22 2125299  
Barua Pepe: [ps@utumishi.go.tz](mailto:ps@utumishi.go.tz)  
Tovuti: [www.utumishi.go.tz](http://www.utumishi.go.tz)



Menejimenti ya Utumishi wa Umma  
Jengo la UTUMISHI  
8 Barabara ya Kivukoni  
S.L.P. 2483  
**11404 DAR ES SALAAM.**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.Na.CCD.273/431/01/C**

**05 Agosti, 2018**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI  
KUHUSU UTEUZI WA MAKATIBU TAWALA WA WILAYA 2018**

**1.0 Utangulizi**

- 1.1 Ndugu wana habari, habarini za asubuhi. Awali ya yote, naomba nitumie fursa hii adhimu kuwashukuru kwa kuacha ratiba zenu na kuitikia wito wangu wa kuja kunisikiliza. Japokuwa leo ni siku ya Jumapili wengi wetu wamepumzika lakini sisi kwetu pamoja na mapumziko, ***Hapa ni Kazi tu!***
- 1.2 Leo nimewaita kuzungumza nanyi kuhusu Uteuzi na Uhamisho wa baadhi ya Makatibu Tawala wa Wilaya. Kwa mamlaka niliyokasimiwa kwa mujibu wa Sheria nimefanya uteuzi wa Makatibu Tawala wa Wilaya ili kujaza nafasi wazi kumi na nane (18) zilizopo katika wilaya za Kinondoni, Mpwapwa, Dodoma, Iringa, Bukoba, Kigoma, Siha, Mtwara, Newala, Misungwi, Njombe, Kondoa, Manyoni, Kilindi, Chunya, Pangani, Bagamoyo na Handeni.
- 1.3 Uwepo wa nafasi hizi umetokana na sababu mbalimbali zikiwemo; kustaafu kazi kwa mujibu wa sheria, kuacha kazi, uhamisho na baadhi ya Makatibu Tawala kupangiwa majukumu mengine

yakiwemo yale ya Ukuu wa Wilaya, Usaidizi wa Katibu Tawala wa Mikoa na yale ya kimuundo.

## 2.0 Makatibu Tawala wa Wilaya wapya na vituo vyao vya kazi

2.1 Makatibu Tawala wa Wilaya walioteuliwa na vituo vyao vya kazi ni kama ifuatavyo;

NA.	JINA	KITUO CHA KAZI	MKOA
1.	Stella Edward Msoffe	Kinondoni	DAR ES SALAAM
2.	Bupe H. Mwakibete	Temeke	DAR ES SALAAM
3.	Sheila Edward Lukuba	Ilala	DAR ES SALAAM
4.	Sara John Komba	Mpwapwa	DODOMA
5.	Zahara Muhidini Michuzi	Chemba	DODOMA
6.	Kodole M. Kiligala	Bukoba	KAGERA
7.	Ally Hassan Mchome	Mwanga	KILIMANJARO
8.	Joseph Paschal Mabiti	Siha	KILIMANJARO
9.	Michombero Anakleth	Chunya	MBEYA
10.	Kasilda Mgeni	Mtwara	MTWARA
11.	Daniel M. Zenda	Newala	MTWARA
12.	Petro Sabato	Misungwi	MWANZA
13.	Emmanuel D. George	Njombe	NJOMBE
14.	Charles Mkama	Manyoni	SINGIDA
15.	Warda Abeid Maulid	Kilindi	TANGA
16.	Hassan Bakari Nyange	Pangani	TANGA
17.	Boniface Maiga Juma	Handeni	TANGA
18.	Hamza Amri Athumani	Bagamoyo	PWANI

## 3.0 Uhamisho

3.1 Aidha ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi nimewahamisha Makatibu Tawala wa Wilaya wanne (4) kutoka katika vituo vyao vya sasa kama ifuatavyo;

- 
- i. **Bw. Hashimu Komba** – Aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Temeke Mkoani Dar es Salaam anahamishwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Iringa, Mkoani Iringa;
  - ii. **Bw. Edward Jonas Mpogolo** – Aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Ilala Mkoani Dar es Salaam anahamishwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Dodoma, Mkoani Dodoma;
  - iii. **Bw. Ally Nyakia Kilukile** – Aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Chemba Mkoani Dodoma anahamishwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kondo, Mkoani Dodoma;
  - iv. **Bw. Yusufu Muhoja Kasuka** - Aliyekuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Mwanga Mkoani Kilimanjaro anahamishwa kuwa Katibu Tawala wa Wilaya ya Kigoma, Mkoani Kigoma.

#### **4.0 Kuripoti**

- 4.1 Makatibu Tawala wa Wilaya Wateule wote hawa wanatakiwa kuripoti katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Dodoma ifikapo tarehe 9 Agosti, 2018 wakiwa na vyeti vyao halisi vya kumaliza kidato cha nne na sita pamoja na vya taaluma zao na nakala za vyeti hivyo zilizothibitishwa kisheria.

**Asanteni kwa kunisikiliza.**

  
Kapt (Mst) George Huruma Mkuchika (MB)

**WAZIRI WA NCHI - OFISI YA RAIS**  
**(MANEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)**